Azimio la Bogota kuhusu
Haki za Ushuru kwa Haki za Wanawake
2017

*** Mashirika yanakaribishwa kutia saini ili kuunga mkono Azimio hili : http://bit.ly/2AtpYE2**

Sisi, washiriki wa kikao cha kwanza cha kimataifa kuhusu haki za ushuru kwa haki za wanawake kutoka tarehe 13-15 Juni, mwaka 2017 jijini Bogota, nchini Colombia, tulikutanika pamoja kama jamii ya kimataifa ya wanawake– mawakili na wahamasishaji, wanasheria na mahakimu, wasomi na wajasiriamali, na wanavyama vya wafanyakazi vya umma- kama sauti ya pamoja ya kutetea haki za ushuru tukiwa na nia ya kuanzisha na kuthibitisha misimamo imara na ya pamoja ya kuunga mkono juhudi za pamoja zinazolenga kubadilisha imani kuhusu haki za ushuru kwa haki za wanawake katika miaka ijayo. Tunatambua na kujitolea kuimarisha suluhu zinazoangazia unyimwaji wa haki za kibinadamu za wanawake kupitia uungwaji mkono wa mifumo ya kiushuru inayorudisha nyuma hali hii na kusababisha ongezeko la umaskini na utengwaji wa wanawake katika uchumi wa ulimwengu.

Tunatoa shukran zetu za dhati kwa Wakfu wa Friedrich Ebert (FES), Mwungano wa Haki za Ushuru Ulimwenguni (GATJ), Mtandao wa Haki za Ushuru (TJN), Ushirika wa Kimataifa wa huduma kwa Umma (PSI), na wabia wetu wa Colombia kwa kuwa wenyeji wa kikao cha kwanza ulimwenguni kuhusu haki za ushuru kwa haki za wanawake kwa kutupa msaada wote uliohitajika.

Tunashukuru na kutambua jukumu na mchango wa jamii ya kimataifa ya wanawake katika kufaulisha kongamano hili, ikiwa ni pamoja na mawasilisho tofauti tofauti, upeperushaji wa habari, mawasiliano kwenye majukwaa ya kijamii na mtandaoni, na ujengaji wa kampeni ya upangaji wa siku za hatua za kimataifa kuhusu haki za ushuru kwa wanawake zilizoendeshwa kwa kushirikiana na Mwungano wa Haki za Ushuru Ulimwenguni (GATJ), Vyama vya wafanyakazi ulimwenguni, na wabia wa mashirika ya kijamii mnamo mwezi Machi 2017.

Tunakumbuka kujitolea kwa viongozi wa ulimwengu, ikiwa ni pamoja na utimizaji wa Ajenda ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mahitimisho yaliyoafikiwa ya Umoja wa Mataifa ya Halmashauri ya Hadhi ya Mwanamke kikao cha 61 (CSW61), Ajenda ya Addis Ababa ya Hatua za Kufadhilia Maendeleo 69/313, ambayo inajukumisha serikali kuchukua hatua za kutenga rasilimali ya kufanikisha shughuli za usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana. Ahadi hizi zinaenda sambamba na Kifungu cha 2.1 cha Agano la Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni la 1976 (ICESCR 1976), ambalo linahitaji kila taifa liendelee kufanikisha haki hizi kwa kuzidi kuongeza rasilimali hadi kufikia upeo unaowezekana.

Pia tumefahamu ya kuwa Azimio la Haki za Kibinadamu kwa Wote (UDHR) linatangaza kuwa ‘kila mtu anafaa kupata (…) haki zote na uhuru wote unaotolewa katika Azimio hili (Kifungu cha 28), bila kubaguliwa kwa misingi ya kijinsia.’ na kuwa Mapatano ya Uondoaji wa kila aina ya Dhuluma dhidi ya Wanawake (CEDAW) yanatambua ‘haki sawa za wanaume na wanawake za kufurahia haki za kiuchumi,

kijamii, kitamaduni, za kiraia na za kisiasa' (utangulizi) na Azimio la Beijing na Jukwaa la Hatua (1995) linalotoa mwito wa uandaaji wa rasilimali katika viwango vya kitaifa na kimataifa kufanikisha maendeleo ya wanawake.

Tunataka marejeleo kamili na ya wazi kwa sera hizi na kwa wajibu huu wa kisheria katika majukumu ya kitaifa na kimataifa ya kuandaa mapato yanayotosha kufikia malengo haya, na kuandaa mapato hayo kwa kupitia sheria taratibu za ushuru ambazo zinatambua na kuboresha haki za wanawake na kutumia mapato hayo kwa njia zinazoondoa mifumo sugu na iliyokita ya kutokuwa na usawa kati ya mume na mke, kupitia kwa upatikanaji wa huduma za umma katika elimu, afya, uangalizi, maji, usafi, usafiri, usalama wa kijamii kwa wote, na baina ya waliotengwa kisiasa na wenye mamlaka, na miongoni mwa mataifa katika viwango tofauti vya maendeleo na uendelevu wa kiuchumi.

Tunatambua changamoto zinazowakumba wanawake katika hali za rasilimali haba ya kugharamia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na utoaji wa huduma kwa umma. Mara nyingi, sauti za wanawake hasisikiki katika mijadala kuhusu sera iliyotawaliwa na mtaji wa ulimwengu. Huku serikali za kitaifa zinaridhia msukumo wa mashirika ya kibiashara kuhusu kupewa nafuu katika ulipaji ushuru, haki za kupata ardhi, maji, na ruzuku ya serikali, huku wakiyapuuza matakwa ya wanawake kuwa mashirika ya kibiashara yatozwe ushuru kwa njia sawa, mahitaji ya wanawake na watu wote wanaohusiana na ustawi wa jamii za kibinadamu yanazidi kupuuzwa.

Tunafahamu kuwa kauli mbio ya 'kutoza ushuru kwa maendeleo' imepigiwa upatu na
Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), na Mwungano wa Ulaya (EU) katika kutoa mapendekezo sawa ya kifedha kwa mataifa yenye mapato ya chini na pia yenye mapato ya juu. Mapendekezo yao ya sera za ushuru yaliyolenga umahsusi wa taifa husika yameegemezwa katika hali za taifa husika, ila fomula ya 'kutoza ushuru kwa maendeleo' imekuwa ni ile ile kila mahali: yaani kuwatoza ushuru watu binafsi na mashirika ya kibiashara yanaoendelea; kupata mapato zaidi kutokana na viwango vya juu 'sawia' vya ushuru wa matumizi kama vile ushuru kandamizi wa VAT na wa bidhaa; kutoa nafuu ya ushuru kwa mapato yatokanayo na uwekezaji, akiba, mapato kutokana na mtaji, na kutoza mifumo ya shughuli za kijamii ili kupunguza bajeti za serikali.

Katika mataifa yenye mapato ya juu, matokeo yamekuwa ni kushuka kwa usawia wa viwango vya ushuru (mapato ya ushuru kama sehemu ya Mapato jumla ya Nchi yaani GDP). Hili limechangia kuendelea kupunguza bajeti za serikali zinazogharamia huduma na mipango za serikali, mipango ya kudumu ya serikali ya kupunguza gharama ambazo wanadhania sio muhimu sana. Katika mataifa yenye mapato ya chini, hata yaliyo na uwiano wa ushuru unaoongezeka, matokeo yamekuwa ni kuongezea utegemezi katika jinsia na ushuru kandamizi wa VAT kwa mapato na ushuru wa bidhaa ambao ni mzigo mkubwa kwa wasio na usalama wa kiuchumi, na upunguzaji wa utumiaji wa ushuru unaokatwa pole pole kutokana na mapato ya watu binafsi na mashirika ya kibiashara ambao unapaswa kutumiwa ili kuongezea mapato ya serikali kutokana na walio na mapato ya juu.

Tunatambua kuwa matokeo ya tawala za 'kutoza ushuru kwa maendeleo' yamekuwa ni kuongezea urundikaji wa mapato na utajiri kwa watu wachache walio matajiri sana na kwa kampuni kubwa kubwa. Upanukaji wa mwanya wa kimapato kati ya ulimwengu wa Kaskazini na wa Kusini, kati ya matajiri na watu wengine, na kati ya wanawake na wanaume imefikia viwango vya kuwa mgogoro katika mataifa husika katika kila kiwango cha maendeleo.

Tunakiri kuwa mataifa yanayoendeshwa kidemokrasia daima yamekuwa yakitegemea mapato kutoka kwa ushuru kama chanzo kikuu cha ufadhili wa kukidhia mahitaji na haki zote za wananchi.

Tuna wasiwasi kuwa:

1. Mgawanyo wa ushuru kwa misingi ya uwezo wa kulipa ushuru, na kwa misingi ya ushuru wa juu unaotozwa pole pole kwa walio na mapato makubwa, umezidi kupuuzwa huku viwango vya juu vya ushuru wa matumizi (ushuru wa nyongeza ya thamani yaani VAT au ushuru wa bidhaa na huduma yaani GST) vimetumika kuchukua nafasi ya viwango vya ushuru vilivyopangwa kwa daraja vinavyotozwa mapato ya juu ya matajiri na mashirika ya kibiashara.
2. Serikali hazijihusishi sana na kufadhilia huduma za elimu, afya na maji kwa wote, na huduma za uangalizi, kutoa ruzuku ya serikali kwa umma na malipo ya uzeeni, na kulinda haki za kimsingi za kiuchumi na kijamii za wanawake wote.
3. Kwa msingi wa fasili ya mashirika ya kibiashara kama 'watu' waliotambulika kisheria walio na haki zote za kisheria za binadamu asili, serikali za kitaifa na taasisi za kifedha za kimataifa zinaruhusu mashirika ya kibiashara kuzurura ulimwengu mzima kwa raha zao huku wakijihodhia kila hisa za ardhi zinazoongezeka thamani, mali ya asili, mapato, na mitaji ya kifedha.
4. Sasa kuna mashirika mengi ya kibiashara kuliko mataifa huru miongoni mwa mia moja bora yenye mapato ya juu kwa mwaka kufikia (2015), na mashirika haya yana mapato bora zaidi kuliko nchi nyingi isipokuwa tu zile chache zilizo tajiri zaidi. Hii ni changamoto ya kweli, kwa sababu, huku wanawake bado wanang'ang'ana kutumia sheria za kikatiba, za haki za kibinadamu, na za kimataifa za haki za kibinadamu ili kupata haki za kupiga kura na nafasi za kuchaguliwa katika serikali za kitaifa, bado wanawake wana nafasi kidogo sana katika masuala ya uongozi serikalini.
5. Wanawake wana uwakilishwaji wa chini zaidi katika umiliki na uongozi wa mashirika ya kibiashara, na huwa ni sheria chache sana za kikatiba, za haki za kibinadamu, na za kimataifa zinazohakikisha kuwa kuna uwakilishwaji sawa katika maendeleo, uwekezaji, na maamuzi ya ulipaji wa ushuru yanayofanywa na kampuni kubwa za kimataifa zinazotengeneza bidhaa, zinatoa malighafi, na mashirika ya kifedha. Huku mitazamo ya mashirika ya kibiashara ikizidi kuathiri uongozi ulimwenguni, nafasi ya wanawake katika ushawishi wa sera inadidimia na kusakamwa zaidi na wakati huo huo maendeleo yao yanazidi kutegemea maamuzi ya uongozi wa mashirika ya kibiashara.
6. Sera za ushuru ambazo zinalenga kikamilifu kuimarisha ukuaji wa kiuchumi zimewezesha na kuzawadia mashirika ya kibiashara yaliyotawaliwa na wanaume, zimewezesha maeneo ya ushuru kuandaa sehemu zisizotozwa ushuru kwa wamiliki matajiri na kwa mashirika ya kibiashara, na kutoa nafasi ya kisheria kwa mashirika haya kujenga mfuatano wa ugavi katika ulegezaji wa ushuru, vifuta jasho vya ushuru wa kibiashara, maeneo maalum ya kiuchumi, na mataifa yatozayo ushuru wa chini. Wakati huo huo, sera za kiushuru zinazowaathiri wanawake, ikiwa ni pamoja na viwango vya juu vya ushuru wa VAT/GST kwa wanawake wenye mapato ya chini hutoa ufadhili haba kwa huduma za umma zinazohitajika kwa maendeleo ya kibinadamu, lakini zinaendelea kuunga mkono kupunguza ushuru unaolipwa na watu wenye mapato manono na biashara.

Tunaamini kuwa

1. Bila mabadiliko muhimu kwenye mifumo ya utozaji ushuru kuinua hatua zinazoongeza usawa na uendelevu wa mifumo ya kifedha inayoafikiana na masilahi ya wanawake, kupungua kwa idadi ya serikali zinazowajibikia raia wake na kuchipuka kwa mashirika ya kibiashara yanayojali maslahi yao wenyewe kutaendelea bila pingamizi yoyote.

2. Ni muhimu sana kwa mashirika ya kimataifa na watu matajiri kulipa sehemu yao ya ushuru, na kwa mataifa yote kukutanika katika meza ya kuamua sera za kimataifa kuhusu ushuru.
3. Bila sera za ushuru unaotozwa hatua kwa hatua, serikali zetu haziwezi kutimiza majukumu yake ya haki za kibinadamu kwa raia wake, na ni wanawake na watoto wanaoumia zaidi wanaponyimwa huduma bora za umma zinazofaa katika elimu, afya, nyumba, kufikia mfumo wa mahakama unaofanya kazi, rasilmali za kuzuia fujo kwa wanawake, kupata maji safi, na choo, na mapato ya kutosha.

Kwa hivyo

Tunahuisha kujitolea kwetu kushirikiana na mashirika yenye washirika wengi pamoja na, ila si tu, Umoja wa Mataifa –UN, wadau wa serikali na wasio wa kiserikali, na pia wadau wote muhimu katika rubaa za kitaifa, kimaeneo na kiulimwengu, ili kuimarisha haki za ushuru kwa haki za wanwake;

Tunakubali kuanzisha vuguvugu la kimataifa la haki za ushuru kwa haki za wanawake likifanya pamoja na Mwungano wa Haki za Ushuru Ulimwenguni (GATJ) na mashirika na mitandao yetu mbali mbali kuimarisha mfumo sawia wa kifedha ulimwenguni unaotetea haki za ushuru, maendeleo endelevu na ukuaji wa uchumi kwa wote.

Kujitolea kuhudhuria vikao vya mara kwa mara vya kimataifa kuhusu haki za ushuru kwa haki za wanawake ili kuunda mikakati pamoja, kutathmini hatua zilizopigwa na kuangazia changamoto ili kufahamu mipango ya harakati za mustakabalini.

Kutoa mwito kwa serikali ili wahakikishe kuwa

1. Athari zote hasi za kijinsia zilizopo katika aina zote za ushuru, matumizi ya fedha, sera za kimataifa, na sheria nyinginezo za kifedha zinafaa kurekebishwa kwa dharura.
2. Hakuna mamlaka ya kisheria yanayofaa kupitisha sheria mpya zozote za ushuru au za matumizi, mipango, au matendo yanayoongeza mapengo ya kijinsia ya mapato.
3. Rasilimali zote zinazopatikana zinatumika vyema kuwekeza katika huduma bora za umma na zinazoafikiana na mahitaji ya jinsia zote, uchumi wa huduma za uangalizi, na ruzuku kwa kijamii. ‘Kutoa ushuru kwa haki za wanawake’ ni mwito wa kuzalisha mapato yanayotosha ili kuongezea uwekezaji wa serikali katika huduma kwa umma kwenye nyanja za elimu, afya, huduma za uangalizi, usafiri, usalama wa chakula, na nyumba ili kupunguza mgao wa kazi bila malipo kwa wanawake na kuongeza mapato ya soko, mapato baada ya ushuru na mamlaka ya kisiasa.
4. Kila kiwango cha serikali huwa kinapanga bajeti zake kulingana na jinsia ili wasiwadhulumu wanawake, kuhakikisha wanawake wana nafasi kushiriki kwa uamuzi wa jinsi pesa za umma zinavyotumika.
5. Mapato yote ya serikali kutokana na ushuru yanapatikana kupitia kwa njia za kuongezeka hatua kwa hatua iwezekanavyo- kupitia kwa kutoza ushuru moja kwa moja kwa mapato, utajiri, na watu binafsi wenye mali nyingi- na kuhakikisha kuwa mashirika ya kibiashara ya kimataifa yanalipa mgao wao wa ushuru. Malipo ya chini ya kiwango kimoja na viwango vya chini vilivyopangwa kwa daraja vya mapato ya watu binafsi na ya mashirika ya kibiashara na ushuru wa mtaji vinafaa mara moja kugeuzwa na kuwa mifumo ya ushuru wa mapato iliyo na viwango vilivyopangiliwa kidaraja- ambao ni mfumo wa kweli wa ushuru ‘unaotozwa pole pole’– ambao msingi wake wa kutoza ushuru ni uwezo wa kulipa kwa walio na mapato ya chini na walio na malipo ya juu.

1. Kutathmini athari za ushuru huwa kunafanywa mara kwa mara- hasa utathmini wa athari hizo kwa wanawake maskini.

2. Sera za kitaifa na kimaeneo kuhusu ushuru na siri za kifedha huwa hazichangii kwa kiwango kikubwa dhuluma za kiushuru katika mataifa mengine na huwa haziegemei kwa mataifa tajiri, mashirika ya kibiashara, au watu walio na mapato ya juu.
3. Serikali za kitaifa pamoja na mashirika ya kimaeneo wanaunga mkono uundwaji wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Ushuru Ulimwenguni ambayo itakuwa shirikishi na yenye uanachama wa serikali za mataifa mengi, ambapo nchi zote, siyo tu zile za G20, zitakuwa na viti sawa katika meza hiyo moja na sauti sawa katika uamuzi wa sera za ushuru wa kimataifa.

1. Mifumo yote ya mapato ya 'ushuru kwa usawa wa kijinsia' iwe na sifa zifuatazo:
    i. Ushuru wa kukatwa pole pole kutoka kwa mapato ya watu binafsi na ya mashirika ya kibiashara yazalishe angalau asilimia 60% ya mapato yote ya nchi;
    ii. Marupurupu ya ziada yatolewe kwa watu wote walio katika kazi za kulipwa wanaopata kiwango cha chini ya mapato-yaliyo-juu ya viwango vya umaskini;
    iii. Nyongeza za mapato huimarisha siyo tu kazi za vibarua au zisizo za kudumu, ila pia kazi nzuri na kudumu zenye mshahara;
    iv. Msamaha wa ushuru huhakikisha kuwa hakuna ushuru wa mapato au ushuru unaochangia huduma za kijamii unaoweza kuwatoza watu ushuru hadi wakabakia maskini;
    v. Viwango vya ushuru unaotozwa kwa mapato huwa vinawezesha serikali kusambaza upya mapato ya masoko kutoka kwa walio na mapato ya juu hadi kwa walio na ya kadiri na ya chini kabisa;
    vi. Hali za gharama ya maisha huwa zinafanya viwango vya ushuru unaotozwa pole pole kutokana na mapato kuwa sambamba ba hali halisi ya gharama za maisha;

    vii. Msamaha wa ushuru huwa ni wa juu kiasi cha kuwa hakuna anayejipia ushuru wa mapato au makato ya ushuru wa kuchangia huduma za umma iwapo mapato yao ni chini ya viwango vya wenye mapato ya chini, na huduma za umma kama chakula, nyumba, elimu, usafiri, na marupurupu ya mapato yanayoweka kila mmoja juu ya viwango vya umaskini;
    viii. Watu wazima wote wanatozwa ushuru kama mtu binafsi na kuhakikisha kuwa manufaa ya ushuru, manufaa ya pesa, na aina yoyote ya huduma za serikali hutolewa kwa wanawake kama watu binafsi ili kulinda uhuru wao wa kifedha;
    ix. Marupurupu yasiyotozwa ushuru yametolewa kwa watoto wanaomtegemea mlipa ushuru kwa miaka yao yote ya masomo shuleni;
    x. Hali zote zinazoleta manufaa ya ushuru badala ya msaada kwa umma au kwa mtu binafsi ziondolewe (yaani kuondoa gharama zote za ushuru, ambazo kwa jumla haziwafikii walio na mapato ya chini).
    xi. Ushuru wote, pesa zote, na manufaa yote yanayotolewa kama msaada ili kutoa ruzuku kwa kazi isiyolipwa kwa wanawake na hivyo kuleta vikwazo vya ushuru kwa kazi ya kulipwa ya wanawake lazima uangaliwe upya;
    xii. Mifumo isiyolegea ya kiushuru (kama ushuru wa kutazamiwa na kushutumiwa) na ushuru usio rasmi na ushuru haramu (kama kodi au malipo yanayodaiwa na wahusika wasiofahamika) yaliyolengwa kwa biashara ndogo ndogo, za pembeni na ambazo si rasmi, iondolewe na nafasi yake kuchukuliwa na ushuru wa chini kwa faida halisi, na miradi ya serikali ya kuwapa uwezo wa kifedha wafanyabiashara dogo dogo.

xiii. Hasa katika mataifa yaliyo na mapato ya chini, upangaji upya mikakati ya usalama wa mapato kama mifumo ya mchango wa moja kwa moja iliyofadhiliwa kwa kiwango kikubwa na waajiri pamoja na serikali kwa wote wasioweza kujiwekea akiba ya mtaji wa kutosha wa kuwapa usalama wa kimapato maishani mwao;

xiv. Kuwazawadia wafanyakazi na biashara zinazoingia kwenye sekta ya uchumi rasmi kwa msaada wa kutegemeka, lakini wazuie matumizi ya sheria za utozaji ushuru zinazowaadhibu na pia hatua kandamizi za uthibiti.

Mashirika yanakaribishwa kutia saini ili kuunga mkono Azimio hili : http://bit.ly/2AtpYE2